

## KIZIDUO CHA

### KMUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA, UTAWALA NA MIPANGO KILICHOFANYIKA TAREHE 23/11/2021 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI.

#### A: WAJUMBE WALIOHUDHURIA

1. Mhe. John I. John	Diwani wa Kata ya Kafita	M/ Kiti
2. Mhe. Mashaka J. Magege	Diwani Kata ya Izunya	Mjumbe
3. Mhe. Agatha A. Malugumba	Diwani wa Kata ya Nyang'hwale	Mjumbe
4. Mhe. John Shilinde	Diwani Kata ya Bukwimba	Mjumbe
5. Mhe. Stella S. Ndege	Diwani V/M Kata ya Nyijundu	Mjumbe
6. Mhe. Revocatus Ng'hwaya	Diwani Kata ya Busolwa	Mjumbe
7. Mhe. Charles Y. Masamyiwa	Diwani Kata ya Kaboha	Mjumbe

#### B: WAJUMBE AMBAO HAWAKUHUDHURIA KWA TAARIFA

1. Mhe. Hussein N. Amar	Mbunge Jimbo la Nyang'hwale	Mjumbe
-------------------------	-----------------------------	--------

#### C: WATAALAMU WALIOHUDHURIA

1. Ndg. Husna T. chambo	Mkurugenzi Mtendaji (W)	Katibu
2. Ndg. David T. Rwazo	Afisa Utumishi na Utawala (W)	
3. Ndg. Andrew Nyanda	Kaimu Afisa Mipango na Ufuatiliaji (W)	
4. Ndg. Patrick Athanas	Afisa Elimu Sekondari (W)	
5. Ndg. Selemani Mgeleka	Kaimu Afisa Elimu Msingi (W)	
6. Ndg. Fabian Yinza	Katibu Tawala (W)	
7. Ndg. Rajab B. Mmunda	Afisa Kilimo Ushirika na Umwagiliaji (W)	
8. Dr. Khadija I. Zaggega	Kaimu Mganga Mkuu (W)	
9. Ndg. Patrick Bayona	Kaimu Afisa Usafi na Mazingira (W)	
10. Ndg. Jesca Magero	Kaimu Afisa Maendeleo ya Jamii (W)	
11. Adv. Shilla S. Mkenka	Kaimu Mwanasheria (W)	
12. Ndg. Abel G. Hau	Kaimu Afisa TEHAMA (W)	
13. Ndg. Dickson Msumari	Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi (W)	
14. Eng. Charles Victor	Kaimu Mhandisi wa Ujenzi (W)	
15. Ndg. Nahshon P.T Magumba	Mratibu wa TASAF	
16. Ndg. Mwasi Bitta	Kaimu Afisa Ujgavi na Manunuzi (W)	
17. Ndg. Peter Mlela	Kaimu Afisa Ardhi na Maliasili (W)	
18. Ndg. Peter Kirei	Kaimu Mweka Hazina (W)	
19. Ndg. Jimmy Rubahindura	Kaimu Afisa Nyuki (W)	
20. Ndg. Syliakus Primu	Kaimu Afisa Usafirishaji (W)	
21. Ndg. David M. Mabula	Afisa Uchaguzi (W)	
1. Ndg. Elimboto Z. Ntandu	Mkaguzi wa Ndani (W)	

#### D: SEKRETARIATI.

1. Ndg. Alex M. Shabo	Mwandishi wa vikao
2. Ndg. Huruma M. Sulusi	Mwandishi wa Vikao

#### KUMB.Na.01/11/2021/2022. Kufungua Kikao

Baada ya akidi kutimia Katibu aliwaeleza wajumbe kuwa hiki ni kikao cha Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango cha kujadili taarifa za kuishia 30, Oktoba 2021, kisha alimkaribisha

Mwenyekiti ili afungue kikao. Mwenyekiti aliwataka wajumbe wajadili hoja kwa umakini kwa kuzingatia sheria taratibu na Kanuni za vikao, alifungua kikao saa 05:10 Asubuhi kwa kuwataka wajumbe wajadili hoja kwa umakini na kwa kutumia muda mfupi.

**KUMB.Na. 02/11/2021/2022. Kuthibitisha Ajenda**

Ajenda zilizothibitishwa na kujadiliwa ni;-

- i. Kufungua kikao
- ii. Kuthibitisha Ajenda za Kikao
- iii. Taarifa ya mapokezi ya fedha Tshs. 1, 080,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 54.
- iv. Kufunga Kikao.

**KUMB.Na. 03/11/2021/2022. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango.**

Muhtasari ulisomwa na ukathibitishwa na wajumbe wa kikao.

**KUMB.Na. 04/11/2021/2022. Taarifa ya mapokezi ya fedha Tshs. 1, 080,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 54.**

Taarifa iliwasilishwa na Kaimu Afisa Mipango (W) na ikapokelewa na wajumbe, wakati anawasilisha alieleza kuwa, Halmashauri imepokea fedha kiasi cha Tshs. 800,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 40 ya shule za Sekondari na kila darasa litatumia kiasi cha Tshs. 20,000,000.00 ikiwa ni pamoja na viti na meza. Kwa upande wa shule za Msingi Halmashauri imepokea jumla ya Tshs. 280,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 14 na kila darasa lita pata kiti na meza ya mwalimu pamoja na madawati 15 ya wanafunzi. Aidha alieleza kuwa utekelezaji wa miradi hiyo unatakiwa kuanza mara moja baada ya kupokea fedha hizo kufikia tarehe 15/12/2021 miradi hiyo iwe imekamilika.

Wajumbe walipokea na kuagiza utekelezaji uanze kufanyika kwa Mhandisi wa ujenzi (W) kuandaa makadirio ya bei (BOQ) kwa ajili ya maandalizi ya kukamilisha miradi hiyo ndani ya muda uliopangwa mara ifikapo tarehe 10/12/2021 miradi hiyo iwe imekamilika na kukabidhiwa kwa wananchi.

**KUMB.Na.11/11/2021/2022. Kufunga Kikao**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa hoja zao za msingi wakati wa kikao na kuagiza yote yaliyojadiliwa yakafanyiwe kazi na utekelezaji wake uonekane katika kikao kijacho. Aidha, Wakuu wa Idara na vitengo wafanye kazi ya ukusanyaji wa mapato kwenye maeneo yao na; Mwanasheria asaidie Halmashauri ili kupata Kamati ya Madini. Pia, Idara ya mipango watoe taarifa ya maendeleo ya miradi ambayo ilishapelekwa fedha. Mwenyekiti ashirikishwe kwenye shughuli mbambali za ukusanyaji wa mapato hasa katika siku zake za ofisi.

Mwisho alisisitiza vikao vifanyike kwa wakati kwa kuzingatia ratiba iwapo kuna dharura wajumbe wataarifiwe mapema ili kuondoa adha na usumbufu usiokuwa wa lazima kwa Wah. Madiwani. Baada ya maelekezo hayo aliahirisha Kikao mnamo majira ya saa 08:50. Mchana.

**MUHTASARI UMETHIBITISHWA**

Katibu



Tarehe

20/12/21

Mwenyekiti



Tarehe

20/12/21